



Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam ni shikira la watu wanaotumia baisikeli kama chombo cha usafiri hapa jijini. Wanachama wetu ni wapanda baisikeli wa kawaida, watu wanaotumia maguta (baisikeli ya gurudumu tatu bila engine), na walemavu wanaotumia baisikeli za mikono.

Tunashukuru kwamba Ferry ya Kigamboni ni huduma nzuri ambayo inategemeka. Ni mara chache sana kwamba hakuna huduma ya ferry. Pia tunashukuru kwamba ferry inatoa kipaumbele kwa wapanda baisikeli na tuna njia maalum kwa wapanda baisikeli kukaa foleni tofauti ya njia ya magari. Aidha, tunashukuru jinsi wanafanyakazi wa ferry wanaangalia na kufuatilia mambo ya usalama wa abiria wa ferry.

Hata hivyo, UWABA tumesikitika kwamba tarehe 1 mwezi wa kwanza 2012, nauli ya baisikeli za guta kuvuka ferry imeongezekwa mara 5, kutoka Tsh 300 mpaka Tsh 1,500 (bila mizigo), na ada za ziada za mizigo kati ya Tsh 200 na Tsh 500. Nauli za magari pia zimeongezekwa, lakini mara mbili siyo mara 5. Pia, magari na pick-up hawalipi ada za ziada za mizigo wakati maguta tunalipa ada hizi. Mpanda guta ambaye anatumia jasho lake kupata mapato ya kila siku analipa Tsh 1,500 hadi Tsh 2,000 kwa kutegemea kiasi cha mizigo. Hii inazidi hata nauli ambayo mwenye gari analipa (Tsh 1,500 ya gari ya kawaida, Tsh 2,000 ya pick up yenye mizigo). Guta haina uzito kama gari kwenye ferry, na pia haitumii nafasi kubwa kwenye ferry kama gari.

Matumizi ya vyombo visivyo vya moto kama baisikeli za maguta yana faida kwa jamii, kwa uchumi na kwa mazingira. Inapunguza uchafuzi wa hewa, haisababishi mabadiliko ya tabia ya nchi, inapunguza kiasi cha mafuta yanaingizwa nchini na inatoa nafasi kwa watu masikini kuongeza kipato kwa kusafirisha bidhaa kwa kutumia nguvu zao bila kununua au kukodi gari. Baba ya Taifa Mwalimu Nyerere alikuwa akitumia baisikeli na kuhamasisha matumizi ya vyombo vya siyo ya moto kama guta kusafirisha bidhaa.

Sera hiyo inaweza kuwa na hasara zifuatazo:

- Bei za bidhaa hasa chakula kwenye soko la Kigamboni zitaongezeka kwa sababu bidhaa nyingi zinasafirishwa na guta
- Wapanda guta watashindwa kulipa nauli hizi na kupoteza biashara, na umasikini wa wapanda guta utaongezeka
- Bidhaa zitasafirishwa na pick-up na vyombo vya moto na siyo na maguta, kwa hiyo uchafuzi wa hewa utaongezeka

Kwa hiyo UWABA tunaomba serikali isikilize maoni ya wapanda baisikeli za guta kwa:

- Kushusha nauli ya ferry ya baisikeli ya guta ya siyo ya engine
- Kuondoa ada za ziada za mizigo kwa maguta (ambazo wenye gari hawalipi)

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

www.uwaba.or.tz

uwabadar@yahoo.co.uk

0713652642, 0715568512, 0713225599